**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE. ZELOTE STEPHEN ZELOTE WAKATI WA MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU 2017 MKOANI RUKWA KIJIJI CHA KIZI WILAYANI NKASI TAREHE 07 APRILI, 2017.**

**Mheshimiwa Meja Jenerali Mstaafu Raphael Muhuga, Mkuu wa Mkoa wa Katavi,**

**Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Ndugu Amour Hamad Amour, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017,**

**Mheshimiwa Eng. Isack Kamwele, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji,**

**Ndugu Wakimbiza Mwenge Kitaifa,**

**Ndugu Wenyeviti wa CCM Mkoa wa Rukwa na Katavi,**

**Ndugu Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa ya Rukwa na Katavi,**

**Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wa Mikoa ya Rukwa na Katavi,**

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

**Viongozi wa Madhehebu ya Dini,**

**Ndugu Wanahabari,**

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa uzima. Aidha napenda kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Rukwa pamoja na viongozi wote mliopo hapa, kwa namna ya kipekee kwa jinsi mlivyojitokeza kwa wingi katika mapokezi ya

Mwenge wetu wa Uhuru 2017 kutoka kwa ndugu zetu wa Mkoa wa Katavi.

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi**

Tunakupongeza kwa kazi kubwa ya kuwasha Mwenge wa Uhuru tarehe 02 Aprili, 2017 na kufanikisha shughuli hiyo ambayo inawakilisha Taifa zima la Tanzania. Hongera sana na hongera wote mlioshirikiana nao na kwa ujumla Wananchi wa Mkoa wa Katavi.

Pia, nakupongeza kwa kuhitimisha mbio za Mwenge wa Uhuru katika Mkoa wako, na kwa kuwatunza Wakimbiza Mwenge Kitaifa katika hali ya usalama.

Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa napenda kukuhakikishia kuwa tutaukimbiza Mwenge wa Uhuru kwa amani, usalama na ari ya hali ya juu.

Wakimbiza Mwenge wote sita wa Kitaifa mliotukabidhi tutawalea, tutawatunza na kuwaenzi na kuhakikisha kuwa wanahitimisha mbio za Mwenge katika mkoa wetu kwa amani, utulivu na mafanikio makubwa.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

Napenda tena kuwakaribisha wewe na Wakimbiza Mwenge Kitaifa katika Mkoa wa Rukwa,

Nasema **KARIBUNI SANA KATIKA MKOA WA RUKWA.**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

Mwenge ukiwa Mkoani Rukwa, utakimbizwa kwa muda wa siku nne katika Wilaya tatu (3) zenye Halmashauri nne (4) ambazo ni:- Halmashauri ya

Wilaya ya Nkasi, Kalambo, Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

Katika kipindi cha siku nne Mwenge wa Uhuru utakimbizwa jumla ya kilomita 749.2 na utatembelea miradi ya maendeleo 43 (kati ya hiyo Sekta ya Elimu 9, Afya 6, Maji 3, Miundombinu 2, Maliasili 5, Kilimo 4, Mifugo 4, Biashara na Viwanda 5) na vikundi 24 (Vijana 13, Wanawake 6, Kundi mchanganyiko 1, Kupambana na Dawa za kulevya 1 na Rushwa 3) miradi hiyo thamani yake ni **Sh.11,793,501,591.00.**

Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kuweka mawe ya msingi, kukaguliwa, kuzinduliwa na mingine kufunguliwa. Mchanganuo wa uchangiaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

a) Wananchi wamechangia jumla ya **Sh.1,545,666,600.00** sawa na asilimia **13.11** ya gharama zote

b) Halmashauri zimechangia **Sh.817,246,745.00** sawa na asilimia **6.93**

c) Serikali Kuu imechangia **Sh.7,796,894,763.00** sawa na asilimia **66.11**

d) Wadau wengine wamechangia **Sh.1,633,693,483.00** sawa na asilimia **13.85**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

Katika kutekeleza Kaulimbiu ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017, Mkoa pamoja na mambo mengine umejikita katika mambo yafuatayo;-

## 1. UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO

Ujumbe Mkuu wa Mwenge wa Uhuru 2017 **"Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu"**

Mkoa wa Rukwa unaungana na Serikali katika kuhamasisha wananchi kushiriki jitihada za Serikali ya Awamu ya tano.

Mkoa umejipanga kwa kutenga maeneo yenye Ekari 2,287 kwa ajili ulipaji fidia na upimaji hadi sasa Ekari 209 zimepimwa kupitia Halmashauri kwa ajili ya shughuli za kukuza uchumi wa viwanda. Mchanganuo wa maeneo kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo:- Nkasi ekari 2023 ambapo ekari 23 ndizo zilizopimwa, Kalambo ekari 41 bado hazijapimwa, Manispaa ya Sumbawanga ekari 186 zimepimwa na zoezi la ugawaji wa viwanja hivyo unaendelea na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ekari 37 ambapo ekari 1 eneo la Kaengesa limepimwa.

## 2. MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA:

Mkoa wa Rukwa unaunga mkono juhudi za Serikali katika Mapambano dhidi ya Rushwa; Chini ya Kauli Mbiu ‘***Tuungane kwa pamoja dhidi ya rushwa kwa maendeleo, amani na usalama wa Taifa letu***’

Kila mwana Rukwa anapaswa kuichukia Rushwa kwani ni adui wa haki, amani na maendeleo yetu. Mkoa kwa kushirikiana na TAKUKURU unafanya jitihada mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio, machapisho mbalimbali, semina pamoja na mikutano ya hadhara. Kupokea malalamiko ya rushwa na kuyashughulikia, kutumia mifumo ya malipo ya kielektroniki ili kuziba mianya ya rushwa na upotevu wa mapato, uanzishwaji wa dawati la malalamiko katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri, usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu za utendaji kazi serikalini. Kwa mwaka 2016/2017 matukio 148 yaliripotiwa TAKUKURU,

kesi 55 zipo kwenye uchunguzi, 11 zipo mahakamani (03 wameshinda 04 wameshindwa).

## 3. MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI:

Mkoa wa Rukwa katika kutekeleza kampeni ya kitaifa ya mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI umeendelea kutekeleza vyema kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru 2017 isemayo Mapambano dhidi ya UKIMWI; chini ya Kauli Mbiu ***Tanzania bila maambukizi mapya, Unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI inawezekana ifikapo mwaka 2030'***

Mkoa umeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutumia mikutano ya hadhara, vikundi vya sanaa, gari la sinema pamoja na semina zinazotolewa na taasisi za kiserikali na sekta binafsi. Vile vile huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa

mtoto (PMTCT) zinaendelea kutolewa katika vituo vya kutolea tiba pia tiba zinatolewa katika Vituo vya Afya kwa wote ambao wana maambukizi ya VVU.

Kiwango cha maambukizi mapya kwa mwaka 2016 inaonesha watu wenye maambukizi ni 4,869 (Me 1,744 sawa na 36% na Ke 3,125 sawa na 64%) sawa na asilimia 2.4% kati ya waliopimwa VVU kwa Mkoa mzima. Mkoa una jumla ya vituo 31 vya kutolea huduma (CTC) ya tiba na malezi kwa wenye maambukizi.

## 4. MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA:

Chini ya kauli mbiu **“‘*Tuwajali na kuwasikiliza watoto na Vijana*’”** Mkoa unaendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya hasa katika makundi ya vijana kwa kutoa elimu ya ujana na ujasiriamali kwa makundi rika.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2017 jumla ya kesi 27 zimefunguliwa polisi ambapo kesi 19 zipo hatua za upelelezi 08 zipo mahakamani (02 za Unga (heroine) 06 za bangi) ambapo kesi 03 zimetolewa hukumu, katika kipindi hicho jumla ya kilo 2.9 za madawa ya kulevya aina ya heroine, Gramu 8,380 za bangi, Miche 510 ya bangi na Jumla ya Ekari 12.5 zimekamatwa na kuteketezwa.

## 5. MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA

Sisi wananchi wa Mkoa wa Rukwa tunaunga mkono mapambano dhidi ya Malaria kwa kauli mbiu ya Mwenge 2017 isemayo '***Shiriki kutokomeza Malaria kabisa, kwa manufaa ya Jamii'***

Mkoa unahimiza wananchi kuweka mazingira yao katika hali ya usafi ili kupunguza mazalia ya mbu waenezao ugonjwa wa Malaria. Mkoa uligawa vyandarua kwenye ngazi ya kaya na katika taasisi

mbalimbali ikiwemo Shule, Hospitali, Magereza na Vituo vya Afya na zahanati, ambapo kwa mwaka 2016 vyandarua 706,079 vilivyotolewa na Red Cross vilisambazwa.

Mkoa wa Rukwa unatoa shukrani za dhati kwa mashirika na taasisi zisizokuwa za kiserikali ambazo tumekuwa tukishirikiana nazo katika mapambano dhidi ya Malaria kupitia mchango wao kwa kusambaza vifaa tiba (MRDT) na vyandarua kwa wananchi pamoja na kutoa elimu ya kujikinga na malaria; Ukusanyaji damu salama na utoaji huduma ya kwanza, kuhamasisha uzazi salama katika ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma. Taasisi hizo ni pamoja na **PSI, Red Cross, Africare na Jhpiego.**

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi**

Baada ya maelezo haya mafupi kuhusiana na mkoa wetu wa Rukwa sasa nipo tayari kuukimbiza

Mwenge wetu wa Uhuru 2017. Tutaukimbiza kwa amani na usalama kuanzia leo tarehe 07 Aprili, 2017 hadi tutakapoukabidhi kwa ndugu zetu wa Mkoa wa Songwe tarehe 11 Aprili, 2017.

Nawasilisha.

**Mwenge Oyeeeeee**